

17 - Al-Qalqalah

قَلْقَلَةٌ Qalqalah – Kugonga

Maana yake kilugha ni kutikisika, kusogea, kutokuwa na utulivu.

Katika hukmu ya Tajwiyd, ni mgongano wa kutetema unaosababishwa na herufi maalum za qalqalah zinapokuwa na sukuwn¹, aidha iwe ya asili au ya kuzuka kwa ajili ya kusimama. Herufi za qalqalah zimekusanyika katika ibara: قَطْبُ جَدِّ

Qalqalah inagawanyika katika daraja mbili

1. القَلْقَلَةُ الكُبْرَى Al-Qalqalatul-Kubraa -Qalqalah Kubwa
Inapokuwa herufi ya qalqalah mwisho wa neno lenye kusimamiwa.
2. القَلْقَلَةُ الصُّغْرَى - Al-Qalqalatus-Sughraa - Qalqalah Ndogo
Inapokuwa herufi ya qalqalah katikati ya neno au mwisho wa neno lakini si neno lenye kusimamiwa.

القَلْقَلَةُ الكُبْرَى Al-Qalqalatul-kubraa (Qalqalah kubwa)	القَلْقَلَةُ الصُّغْرَى Al-Qalqalatus-sughraa (Qalqalah ndogo)	Herufi
وَتَصَدَّقَ	لَوْقَعْتَهَا	ق
تُشَطِّطُ	مَطَّلَعِ	ط
يُعَقِّبُ	عَبْدِهِ	ب
فَأَخْرَجَ	أَجْمَعُونَ	ج
وَيَحْتَلِدُ	فَادَّعُوا	د

¹Imeshaelezwa kwa kifupi katika mlango wa 'Swiffah za Herufi'